**Mapendekezo ya Kimpito ya COVID-19 ya Vituo vya Kusindika Vyakula Yaliyofanyiwa Mabadiliko kutokana na Mapendekezo ya CDC/NIOSH**
**Aprili 20, 2020**

**Utangulizi**
COVID-19 inaweza kusambaa kwa urahisi kwenye sehemu ambapo watu wanafanya kazi kwa karibu sana, kama vile vituo vya kusindika vyakula. Wamiliki, wasimamizi wa vituo, na wanaosimamia wafanyakazi wanafaa kutekeleza mipango ya kupunguza kuwa karibu na virusi vinavyosababisha COVID-19 ili kuzuia usambazaji wa maradhi miongoni mwa wafanyakazi wa kituo. Watu wenye umri wa zaidi ya miaka 65 na watu wenye matatizo yaliyoko awali ya afya kama vile kisukari, maradhi makali ya mapafu na moyo, au wale wenye kasoro ya mfumo wa kinga mwilini (k.v. saratani au kutumia dawa zinazodhibiti kinga mwilini) wako kwenye hatari zaidi ya kuwa wagonjwa sana kutokana na COVID-19. Matatizo ya uambukizi wa COVID-19 yanajumuisha kuhitaji kulazwa hospitalini, kupokea kisaidia upumuaji cha kiufundi na kifo.

Mapendekezo haya ya kimpito yaliundwa kwa maelezo kutoka kwa Taasisi ya Kitaifa ya Afya na Usalama Kazini (NIOSH) na yamefanyiwa mabadiliko kidogo ili yatumiwe kwenye Karolina Kaskazini na Idara ya Kilimo na Huduma za Wateja (NCDA&CS) na Idara ya Afya na Huduma za Binadamu (NCDHHS). Yatasasishwa pale maelezo mapya yanapopatikana. Mapendekezo yananuiwa kuzuia kuwa karibu na COVID-19, inapowezekana, na kulinda afya ya jamii za Karolina Kaskazini ambazo zinajumuisha kikosi hiki muhimu cha wafanyakazi. Viwanda vya kusindika vyakula ni biashara muhimu na inafanya kazi muhimu ili kuhakikisha kuwepo kwa ufikishaji endelevu wa vyakula salama na vyenye kudumisha afya. Mapendekezo haya yananuiwa kuwapatia wasimamizi fursa ambazo kupitia fursa hizo, usalama wa wafanyakazi unaweza kukuzwa. Hayanuiwi kuchukua nafasi ya mipango yoyote iliyopo ya afya na usalama wa wafanyakazi kwenye masharti ya Idara ya Wafanyakazi ya NC (NCDOL), lakini yanafaa kuchukuliwa kuwa yanaongezwa kwenye masharti hayo.

Vituo vya kusindika vyakula kwenye NC kihistoria vimedhibitiwa na NCDOL kuhusiana na majanga ya viwanda, na Idara ya Marekani ya Kilimo -Huduma ya Ukaguzi na Usalama wa Vyakula (USDA-FSIS) na NCDA&CS kuhusiana na usafi na usalama wa vyakula. Hivi karibuni, misambazo ya COVID-19 kwenye vituo ndani ya majimbo mengine, na sasa NC, imehitaji kuundwa kwa mwongozo wa aina mpya ya janga (usambazaji wa virusi vya upumuaji kutoka kwa mfanyakazi mmoja hadi mwingine) ambao haujatambuliwa kihistoria kwenye vituo hivi. Baada ya kupokea maelezo kutoka kwa CDC-NIOSH, Idara ya Afya ya Umma ya NCDHHS na NCDA&CS zimeunda kwa upesi mwongozo huu ili kujaribu kusaidia vituo vya kusindika vyakula.

Vijenzi muhimu vya mpango wa uzuiaji kwa wafanyakazi wa kusindika nyama vinajumuisha 1) kupunguza hatari ya kuwa karibu na virusi, 2) ugunduzi mapema wa watu wenye dalili za COVID-19, na 3) kutenga visa chanya au vinavyoshukiwa viwe mbali na wengine ili wasiweze tena kuambukiza.

**Unda Mpango wa Kudhibiti Uambukizi wa COVID-19**
**Kupunguza kiasi cha msambazo wa maradhi na kuendeleza shughuli kunahitaji kujitayarisha na kutekeleza mabadiliko kwenye kiwanda.**

- Tambua waratibu wa kazini wa masuala ya COVID-19
- Teua mratibu wa uzima kazini ili kufuata itifaki za uzima zilizofafanuliwa hapo chini
- Amua jinsi utakavyofanya shughuli na wafanyakazi waliopungua
- Tekeleza mipango ya kuendeleza shughuli muhimu kwenye biashara yako
- Idhinisha sera nyumbulifu za kazini na za fursa kazini zenye mishahara ambazo ni sawia kwa wafanyakazi wote
- Wapatie mafunzo mseto wafanyakazi ili waweze kutekeleza shughuli muhimu na kudumisha shughuli
- Tekeleza mabadiliko ya kimfumo ili kuunda nafasi na vilinzi baina ya wafanyakazi
- Tekeleza utendakazi bainifu wa kutakasa kwenye sehemu zote za kiwanda
- Tenga makao ya upweke kwa wafanyakazi wenye dalili ambao ni lazima wajitenge na wengine lakini hawawezi kujitenga nyumbani
- Unda mpango wa mawasiliano wa kushiriki maelezo kila siku ili kuimarisha ujumbe wa kielimu, kutoa maelezo yaliyosasishwa kuhusu idadi ya visa vilivyothibitishwa kwenye kiwanda, na kushiriki maelezo kuhusu hatua za kuchukuliwa ili kudumisha usalama wa wafanyakazi, ikiwemo vipimo na ufuatilizi wa mwingiliano

**Tekeleza tathmini za kazini ili kutambua mikakati ya uzuiaji na hatari za COVID-19.**

- Mbali na sehemu za kazini, maeneo mengine ya kuzingatiwa pia yanajumuisha usafiri hadi au kutoka kwenye kituo cha kazini, chumba cha mapumziko kwa wafanyakazi, mkahawa, vyumba vya makabati, vyumba vya vifaa, vyumba vya kuwasili, njia za kuingia na kutoka kwenye maeneo ya kazini, na maeneo sawia
- Zana za ulinzi wa kibinafsi (PPE), ambazo zimetambuliwa kuwa zinahitajika kwenye tathmini hizi, zinafaa kufikishwa na wasimamizi na kubadilishwa inapohitajika (kwa mfano, zinapokuwa chafu au zinapokuwa na vidudu)
- Kisafisha mikono chenye alkoholi na sabuni ya mikono zinafaa kupewa waajiriwa ili zitumiwe

**Fuata Mwongozo wa Kimpito wa CDC – Kutekeleza Utendakazi Salama kwa Wafanyakazi wa Miundombinu Muhimu Ambao Huenda Wakawa Wamemkaribia Mtu Aliyethibitishwa au Anayeshukiwa kuwa ana COVID-19** www.cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/community/critical-workers/implementing-safety-practices.html Tazama tovuti ili kupata maelezo – vidokezo muhimu vimechaguliwa hapo chini:

- Kagua awaili wafanyakazi ili kujua kama wana homa (>100.4 F) na dalili kabla ya kuanza kazi na kabla ya kuingia kwenye usafiri wa kiwanda kama vile matatu na mabasi
- Wafanyakazi wanafaa kuripoti kwa wasimamizi papo hapo wakishikwa na hamu wakati wa awamu yao ya kazi
- Wafanyakazi wenye homa hawafai kufanya kazi na wanafaa kuelekezwa kwenye ukaguzi wa kimatibabu na labda pia kipimo cha COVID–19
- Wafanyakazi wenye homa wanafaa kufahamishwa kuwa wanafamilia wao na walio karibu sana nao pia huenda wakatathminiwa ili kuangalia kama wana dalili
- Wafanyakazi wenye matatizo ya kupumua au wasioweza kusimama kivyao wanafaa kuhudumiwa papo hapo kwa kupiga simu kwa nambari 911 na kuripoti kisa kinachoshukiwa cha COVID-19 chenye dalili kali
- Wafanyakazi wanaoshurutishwa wasiende kazini hivi wanafaa kupata fursa kazini zenye mshahara mpaka matokeo yapatikane na wakati wanapotengwa ikiwa watapata matokeo

chanya

- Wafanyakazi wanafaa kuvaa barakoa ili kufinika pua na mdomo.
- Dumisha masafa ya kijamii vile iwezekanavyo kazini – tazama kifungu cha hapo chini
- Takasa na safisha sehemu za kufanya kazi – tazama kifungu cha hapo chini
- Kuhusu maswala ya kurudi kazini na kuendelea na kazi kwa wafanyakazi binafsi:
    - Kwa wafanyakazi ambao huenda wakawa wamekaribia COVID-19: www.cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/downloads/Essential-Critical-Workers_Dos-and-Donts.pdf

    - Kwa wafanyakazi ambao walikuwa wagonjwa na ni lazima warudi kazini:
        - Mkakati usiotegemea kupima. Asiende kazini hadi:
            - Angalau siku 3 (masaa 72) yamepita *tangu kupona,* ambayo inafafanuliwa kama kutokuwa na homa bila kuhusisha dawa za kupunguza homa na kupungua kwa dalili za upumuaji (k.v. kikohozi, matatizo ya kupumua); na,
            - Angalau siku 7 zimepita *tangu dalili zilipojitokeza kwa mara ya kwanza*
- Wafanyakazi wanaoshurutishwa wasiende kazini wanafaa kupewa fursa kazini zenye mishahara kwa muda wa kushurutishwa wasiende kazini

**Ufuatilizi wa Mwingiliano**

- Ufuatilizi wa mwingiliano unafaa kutekelezwa kwa visa vyovyote vinavyotambuliwa. Hii itakuwa shughuli jumuishi ya mashirika ya jimbo na kienyeji ya afya na usalama wa wafanyakazi au ajira ya kampuni. Kwa ajili wafanyakazi huenda wakakaribia virusi kazini na nyumbani kwao, ni muhimu mashirika ya kibinafsi na ya kibiashara yashirikiane kwenye shughuli hii

**Fuata daraja za vidhibiti wakati wa kutekeleza utendakazi wa kudhibiti uambukizi hasa kwa vituo, na jumuisha mchanganyiko wa vidhibiti vilivyodokezwa hapo chini**

*Vidhibiti vya uhandisi*

- Badilisha vituo vya kufanya kazi ili kupunguza mwingiliano wa karibu baina ya wafanyakazi na wafanyakazi wengine
    - Sakinisha ngao au vilinzi vinavyopenyeza mwangaza inapowezekana
- Tumia mbinu za kuwatenganisha wafanyakazi kwenye maeneo yote ya vituo mbali na maeneo ya kufanya kazi, yakiwemo vyumba vya mapumziko, sehemu za kuegesha magari, na maeneo ya kuingia/kutoka
    - Tekeleza utendakazi kama vile vipengee vya kuonekana (k.v. akama kwenye sakafu, ishara), mahema au makao mengine ya kwa muda
- Ikiwa feni zinatumiwa kwenye vituo, hakikisha kuwa feni zinavuvia hewa safi kwenye sehemu ya upumuaji ya wafanyakazi

*Usafi/Uuaji Vidudu/Utakasaji*

- Tumia kiua vidudu kwenye maeneo yanayoguswa sana ndani ya maeneo ya kuzalisha vyakula kwa kutumia bidhaa zinazokidhi vigezo vya Wakala ya Ulinzi wa Mazingira (EPA) vya kutumiwa dhidi ya SARS-CoV-2 na zilizoidhinishwa chini ya taratibu wastani za shughuli za utakasaji wa kituo
- Ratibu matumizi ya nyenzo ya kusafisha na USDA ikiwa inatumiwa kwenye maeneo ya kuzalisha vyakula
- Kwa maeneo mengine yanayoguswa sana, tumia bidhaa zinazokidhi vigezo vya EPA, michanganyiko hafifu ya blichi ya nyumbani yenye angalau 70% ya alkoholi, na ambayo ni mwafaka ili kutakasa sehemu
- Ikiwa vifaa vinatumiwa na wafanyakazi kadhaa – takasa baina ya matumizi yanayoshirikiwa
- Tekeleza usafishaji wa mara nyingi zaidi unaolenga maeneo yanayoguswa sana ya sehemu zinazoshirikiwa (k.v. saa, sehemu za bafu, meza na viti vya chumba cha mapumziko, mashine za kununua kwa mapeni, viegemeo, vishikio vya milango)

*Vidhibiti vya usimamizi*

- Ukaguzi wa wafanyakazi – tazama kifungu cha hapo juu
- Punguza wafanyakazi kwenye mlolongo wa uzalishaji kiwandani kwa kiwango kiwezekanacho ili kupunguza mwingiliano wa karibu wa wafanyakazi - zingatia kasi ya mlolongo kuwa ni sababu muhimu kwenye haya
- Badili awamu za kazi, nyakati za kuanza na nyakati za mapumziko vile iwezekanavyo
- Wapatie wafanyakazi muda mwafaka na uwezo wa kufikia sabuni, maji, na tauli za kutumiwa mara moja ili waoshe mikono
- Tumia viyoyozi bila mguzo inapowezekana
- Tumia visafishaji mkono vyenye alkoholi vinavyojumuisha angalau 60% ya alkoholi ikiwa sabuni/maji hazipatikani

*Zana za Ulinzi wa Kibinafsi (PPE) na Udhibiti wa Vyanzo*

- Wafanyakazi wanafaa kuendelea kupewa na kuvaa PPE zinazohitajika kwa shughuli za kazi zinazotekelezwa
- Tumia barakoa kama ilivyodokezwa hapo juu, ibadilishe inapokuwa chafu au inapopatikana na virusi
- Sisitiza njia mwafaka ya kuvaa na kuvua vipengee kama vile barakoa ili kupunguza kuwa chafu au kupatikana na virusi
- Sisitiza usafi mwafaka wa mikono baada ya glovu na vinavyofunika uso kuondolewa

**Toa maelezo ya kudhibiti uambukizi na mafunzo kwa wafanyakazi wote**

- Mawasiliano/mafunzo yanafaa kuwa rahisi kuelewa, kwa lugha mwafaka inayopendwa kuongewa na kusomwa na wafanyakazi, na pia yanafaa kujumuisha maelezo sahihi kwa muda mwafaka
- Mada zinajumuisha, lakini haziwekewi kikomo kwa: kubakia nyumbani unapokuwa na homa, kutengana kijamii, PPE, utendakazi wa usafi wa mikono, njia zinazoweza kuambukiza (na jinsi ya kuzipunguza) kwenye jamii